# MTAALA REKEBIFU WA ELIMU YA MSINGI KWA WANAFUNZI WENYE UZIWIKUTOONA

## HATUA YA I-III

## 2021

# Utangulizi

## Usuli


Mtaala Rekebifu wa Elimu ya Msingi kwa Mwanafunzi mwenye Uziwikutoona umeandaliwa kwa kuzingatia sera na matamko mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa kama vile; Tamko la Haki za Binadamu la Mwaka 1948, Tamko la Haki ya Mtoto la Mwaka 1989, Tamko la Kimataifa la Elimu kwa Wote la Jomtien la mwaka 1990, Tamko la Utoaji wa Fursa Sawa kwa Watu wenye Ulemavu la mwaka 1993, Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemavu la Mwaka 2006, Mkataba wa Marrakesh wa Mwaka 2016 unaohusu kuondoa vikwazo katika utoaji wa elimu kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu, Tamko la Salamanka kuhusu utoaji wa elimu maalumu la mwaka 1994, Tamko la Dakar kuhusu utoaji wa elimu kwa wote la mwaka 2000 na Tamko la Elimu Jumuishi la mwaka 2001. Pia, muktadha wa mtaala huu umezingatia makubaliano kuhusu Haki za Watu wenye Ulemavu ya Mwaka 2006, Mkataba wa Haki ya Mtoto wa Afrika wa Mwaka 1990, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Sera ya Taifa kuhusu Ulemavu ya Mwaka 2004, Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa Mwaka 2009-2017, Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa Mwaka 2018-2021, na Sheria Namba 9 ya watu wenye Ulemavu ya Mwaka 2010. Kwa ujumla wake, mikataba ya kimataifa, mipango ya kitaifa, na sera za kitaifa zinaonesha umuhimu wa utoaji elimu kwa watoto wote ikiwa ni pamoja na wanafunzi mwenye mahitaji maalumu, wakiwamo wanafunzi wenye uziwikutoona.

Kuanzia Mwaka 2009, Tanzania imekuwa ikitekeleza mikakati ya elimu jumuishi kwa lengo la kujenga jamii inayozingatia usawa katika utoaji wa elimu kwa wote. Taarifa na utafiti umekuwa ukionesha ubutu katika utekelezaji wa utoaji wa haki ya elimu kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona. Kutokana na changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wenye ulemavu wengi wao wamekuwa wakikosa fursa ya kupata elimu bora na wengine kukosa kabisa. Ripoti ya UNICEF ya mwaka 2018 kuhusu watoto walio nje ya mfumo wa elimu inakadiria kuwapo kwa watoto 400,000 wenye aina mbalimbali za ulemavu wanaostahili kuwa shuleni. Hata hivyo, ni watoto 42,783 (11%) tu miongoni mwa 400,000 walioandikishwa shuleni. Vilevile, utafiti wa Taifa wa mwaka 2008-2009 kuhusu viwango vya ulemavu unaonesha kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi katika shule za msingi

kuwa ni 81.8%, na kwa watoto wenye ulemavu ni 57.6% na watoto wasio na ulemavu ni 82.3%.

Aidha, WyEST inaonesha takwimu za wanafunzi wenye uziwikutoona walioandikishwa shuleni kuanzia mwaka 2012 hadi mwaka 2020.Takwimu halisi zinaoneshwa katika kielelezo kifuatacho.

Jedwali: Idadi ya wanafunzi wenye uziwikutoona katika elimu ya awali na msingi.




wanafunzi wenye uziwikutoona ili waweze kujifunza vyema katika madarasa jumuishi na madarasa maalumu kwa wale wanaoshindwa kumudu stadi za Hatua ya I na Hatua ya II zinazowawezesha kujiunga katika madarasa jumuishi ya elimu ya msingi. Katika utekelezaji wa utoaji elimu ya msingi inayozingatia usawa na ushirikishwaji katika elimu, ni muhimu kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi katika kuwezesha ujenzi wa umahiri. Hivyo, mtaala huu ni rekebifu ili kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona aliyeandikishwa katika shule ya msingi ndani ya kipindi kisichozidi miaka mitatu kujenga umahiri wa mawasiliano, kujimudu na stadi za KKK utakaomwezesha kujiunga na Elimu ya Msingi. Endapo hataweza kumudu vyema umahiri wa kumwezesha kuendelea na elimu ya msingi ataendelea na mtaala rekebifu, sehemu ya pili ambayo inajumuisha ujenzi wa stadi za kujimudu, KKK pamoja na ujasiriamali katika uzalishaji mali, michezo na sanaa, na TEHAMA.

## Historia ya Elimu Maalumu Tanzania

Elimu maalumu ilianza rasmi nchini Tanzania mwaka 1950, ilianzishwa na wamisionari wa mashirika mbalimbali ya dini kutoka Ulaya. Wamisionari hao walianzisha shule na vitengo vya elimu maalumu ili kutoa elimu kwa wanafunzi wenye ulemavu. Hivyo, elimu ilitolewa kulingana na aina ya ulemavu alionao mwanafunzi.

Shirika la Wamisionari wa Kanisa la Anglikana, lilianzisha shule ya msingi ya kwanza kwa wanafunzi wenye ulemavu wa uoni iitwayo Buigiri iliyopo Jijini Dodoma, mwaka 1950. Aidha, Wamisionari wa Kikatoliki wa Uholanzi “White Fathers” walianzisha shule ya wanafunzi wenye uziwi inayoitwa Tabora Viziwi iliyopo Mkoani Tabora, mwaka 1962. Halikadhalika, Wamisionari wa Jeshi la Wokovu walianzisha shule ya msingi kwa wanafunzi wenye ulemavu wa viungo iitwayo Jeshi la Wokovu Jijini Dar es Salaam, mwaka 1967. Vilevile, mwaka 1975 Serikali, kupitia Wizara ya Elimu na Utamaduni wakati huo ilianza kutoa mafunzo ya kuandaa walimu wa elimu maalumu katika fani ya uoni na uziwi. Vilele, mwaka 1984 mafunzo ya walimu wa elimu maalumu katika fani ya kufundisha wanafunzi wenye ulemavu wa akili yalianzishwa.

Kutokana na mwaka 1981 kutangazwa kuwa mwaka wa watu wenye ulemavu duniani, serikali kupitia Wizara ya Elimu na Utamaduni (wakati huo) iliendelea kuanzisha shule na vitengo vya wanafunzi wenye ulemavu.Shule ya kwanza kwa wanafunzi wenye ulemavu wa akili ilianzishwa mwaka 1982 na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara. Vilevile, mwaka 1992 kitengo cha kuhudumia watoto wenye mtindio wa ubongo kilianzishwa jijini Dar es Saalam na Chama cha Kuhudumia Watoto wenye Ulemavu wa Akili na Mtindio wa Ubongo. Hali kadhalika, elimu ya msingi kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona ilianza kutolewa katika Shule ya Msingi Uhuru Mchanganyiko katika jiji la Dar es Salaam mwaka 1993.

Aidha, walimu wenye taaluma ya elimu maalumu walihitajika ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu. Hivyo, ikumbukwe kuwa lengo la kuanzishwa kwa mfumo wa elimu maalumu lilikuwa ni kutekeleza haki za utoaji wa elimu kwa wote ikiwa ni pamoja na watu wenye mahitaji maalumu ya elimu. Aidha, utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye ulemavu ulilenga kujenga uwezo wa kujitegemea na kuondokana na unyanyapaa ulioambatana na maneno ya kudhalilisha utu yaliyokuwa yakitumika kuwatambulisha watu wenye ulemavu kama vile; viwete, vipofu, mataahira na hatimaye kuleta mabadiliko ya

kutumia lugha inayotanguliza utu kwa kutumia majina kama vile; watu wenye ulemavu wa viungo, wasioona na watu wenye ulemavu wa akili. Aidha, lengo lingine lilikuwa ni kutoa huduma za elimu kwa ufanisi na weledi ili kuwafikia watu wengi zaidi na makundi yote ya watu wenye mahitaji maalumu katika mazingira fikivu yaliyoko kwenye maeneo wanakoishi.

Tafiti zimeonesha kuwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu wamekuwa wakiongezeka hivyo kuhitaji mfumo wa elimu unaozingatia mahitaji maalumu ya elimu kwa kila mwanafunzi. Wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu hujumuisha wenye ulemavu, vipawa na vipaji maalumu, usonji na changamoto za kipekee za ujifunzaji; mfano wa changamoto hizo ni kama zile zilizopo katika usomaji (dislekisia), kuandika (disigrafia) na hisabati (disikalikulia). Pia, changamoto za kiafya kama vile; magonjwa ya pumu, selimundu na UKIMWI, pamoja na za kihisia, kijamii na kitabia. Kundi lingine la wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya elimu ni wale wenye changamoto nyingine kama wanafunzi wasio na makazi na yatima. Ili makundi haya ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu yaweze kushiriki kikamilifu katika kujifunza ilionekana wazi kuna umuhimu wa kuanzisha elimu jumuishi hapa nchini.

Tanzania ilianza kutekeleza mfumo wa elimu jumuishi mwaka 1997. Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni “UNESCO” iliandaa mwongozo uliotumika katika kuwawezesha walimu watakaofundisha madarasa jumuishi. Mwaka 1998 shule jumuishi za kwanza za Wailes na Kibasila katika wilaya ya Temeke Jijini Dar es Salaam zilianza utekelezaji wa elimu jumuishi. Wizara ya Elimu na Utamaduni iliendesha mafunzo kwa walimu na wasimamizi wa shule za msingi katika halmashauri zipatazo 76 hapa nchini. Mwaka 2013, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (WyEMU) kwa kushirikiana na Shirika la kuhudumia watoto “UNICEF”, UNESCO, na TET vilihuisha na kutafsiri vivunge vya kufundishia mafunzo ya elimu jumuishi hususani kwa walimu wa shule za awali na msingi, wazazi na wadau wengine wa elimu.

Mwaka 2009 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliandaa Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa mwaka 2009-2017. Baada ya mkakati huo kumalizika, mkakati wa pili wa elimu jumuishi 2018-2021 ulitayarishwa na utekelezaji wake unaendelea. Mkakati huu, unatoa fursa sawa kwa wanafunzi wote kwa kuzingatia mahitaji anuai ya ufundishaji na

ujifunzaji. Aidha, kumekuwa na utayarishaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, mazingira fikivu, njia na mbinu za kufundishia na kujifunzia, mtaala rekebifu na unaozingatia uwapo wa walimu wataalamu na jumuishi.

## Historia ya Elimu kwa Wanafunzi wenye Uziwikutoona Tanzania

Elimu kwa wanafunzi wenye uziwikutoona ilianza mwaka 1993 katika kitengo cha elimu maalumu katika Shule ya Msingi Uhuru Mchanganyiko iliyoko Jijini Dar es Salaam. Kitengo cha wanafunzi wenye uziwikutoona kilianza kwa kuandikisha wanafunzi wawili, mvulana mmoja na msichana mmoja. Darasa la kwanza la wanafunzi hawa wawili wenye uziwikutoona lilianzia ofisini. Mwalimu Medrine Gambo na Anjelica Mtwale ndiyo walikuwa walimu wa kwanza wa wanafunzi hao. Mwaka 1994 waliongezeka wanafunzi wenye uziwikutoona wavulana wawili na ndipo darasa rasmi lilifunguliwa kwa ufadhili wa shirika lisilo la kiserikali la “Solidality Human Rights Inclusion and Accessibility (SHIA)” kwa kushirikiana na serikali chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (wakati huo).

Ushirikiano kati ya Serikali na mashirika ya SHIA na “Christoffel-Blindenmission (CBM)” walianzisha vitengo viwili (2) vya kufundisha wanafunzi wenye uziwikutoona mwaka 2005 katika Shule ya Msingi Iringa Viziwi na Shule ya Msingi Mugeza Viziwi. Huduma hizi za uanzishwaji wa vitengo ulikwenda sanjari na mpango wa kuwaandaa walimu kwa njia ya semina za mafunzo kazini ili waweze kumudu ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wenye uziwikutoona kwa ushirikiano na shirika la “Perkins International” la Marekani.
Mwaka 2006, Shirika la SHIA lilikabidhi jukumu la kuhudumia watoto wenye uziwi kutoona kwa shirika la “Sense International Tanzania (SITZ)” na kuendelea kushirikiana na serikali katika utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye uziwikutoona.

Shirika hili lilishirikiana na TET kuanza mchakato wa kupata mtaala kwa ajili ya wanafunzi wenye uziwikutoona. Aidha, mwaka 2010 TET kwa kushirikiana na SITZ walifanya utafiti ili kubaini uhitaji wa mtaala kwa ajili ya wanafunzi wenye uziwikutoona. Matokeo yalionesha kuwapo kwa uhitaji huo kwani kila kitengo kilionekana kufundisha maudhui ya aina tofauti kulingana na uwezo na ujuzi wa mwalimu. TET kwa ufadhili wa SITZ ilianza mchakato wa kuandaa mtaala, muhtasari na mwongozo rekebifu wa kufundishia wanafunzi wenye uziwikutoona mwaka 2021. Utafiti huu, ulibaini kuwa mtaala unahitaji kufanyiwa marekebisho ili uendane na mahitaji ya wanafunzi wenye uziwikutoona.

Hii ilitokana na uwapo wa mtaala wa elimu msingi wenye taarifa muhimu kuhusu mahitaji maalumu kwa wanafunzi. Hivyo, ilibainika kuwa uhitaji kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona ni mtaala, muhtasari na mwongozo rekebifu utakaomwezesha mwalimu kujenga umahiri katika elimu ya msingi kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona.

Shirika la SITZ liliendelea kushirikiana na Serikali katika kuongeza vitengo hivyo hadi kufikia vitengo 10 vya wanafunzi wenye uziwikutoona mwaka 2013. Aidha, shirika la SITZ limekuwa likishirikiana na Shirika la "Perkins International" katika kuwajengea walimu na walimu mwega uwezo na ujuzi katika utoaji wa huduma ya elimu kwa wanafunzi wenye uziwikutoona. Vitengo hivyo ni; Shule ya Msingi Uhuru Mchanganyiko (Dar es Salaam), Shule ya Msingi Mugeza Viziwi (Bukoba), Shule ya Msingi Viziwi (Iringa), Shule ya Msingi Mwanga Viziwi (Kilimanjaro), Shule ya Msingi Buguruni Viziwi (Dar es Salaam), Shule ya Msingi Masasi Mchanganyiko (Lindi), Shule ya Msingi Msandaka Viziwi (Kilimanjaro), Shule ya Msingi Dongobesh Viziwi (Manyara), Shule ya Msingi Njombe Viziwi (Njombe) na Shule ya Msingi Tumaini Viziwi (Singida).

## Muktadha wa Mtaala Rekebifu wa Elimu ya Msingi kwa Mwanafunzi mwenye Uziwikutoona

Mtaala huu rekebifu wa elimu ya msingi kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona, umeandaliwa katika muktadha wa kuhakikisha utoaji wa elimu bora inayokidhi mahitaji ya sasa ya Mtanzania na yenye kutoa fursa sawa za kujifunza kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona. Mtaala huu umezingatia masuala mbalimbali ikiwamo utekelezaji wa elimu jumuishi, stadi za karne ya 21, kukua kwa sayansi na teknolojia ya habari na mawasiliano, utandawazi, na utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030. Hivyo, mtaala huu rekebifu ni nyenzo mojawapo katika utekelezaji wa lengo la nne (4) la Malengo ya Maendeleo Endelevu linalosisitiza kumwezesha kila mtu kupata elimu na kuhakikisha kwamba binadamu wote wanafikia uwezo wao juu wa kielimu. Mtaala rekebifu unalenga kuhakikisha kuwa Elimu ya Msingi inatolewa kwa ubora na inawanufaisha walengwa ikiwa ni pamoja na wanafunzi wenye uziwikutoona.

Elimu ya Msingi inalenga kuwapata wahitimu ambao ni wazalendo, wanaojitegemea na wenye uwezo wa kushiriki katika shughuli za kijamii na kiuchumi. Wahitimu wa elimu ya msingi wanatarajiwa kuwa ni wenye maarifa na stadi mbalimbali zitakazowawezesha kuchangia katika ujenzi wa jamii jumuishi, yenye amani, na inayojihusisha katika kujenga uchumi wa mtu binafsi na jamii nzima kwa ajili ya maendeleo endelevu. Pia, mtaala huu

unasisitiza utoaji wa elimu jumuishi, yaani elimu inayothamini na kuheshimu uwezo, mahitaji, jinsia na kutambua kwamba wanafunzi wote wanaweza kujifunza na kufanikiwa. Mtaala huu, unatarajiwa kukidhi matakwa ya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa kumwandaa mwanafunzi mwenye uziwikutoona wa Tanzania kuishi katika ulimwengu wenye ushindani.

Mtaala rekebifu umeandaliwa kwa kufuata muktadha wa elimu ya msingi kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona ili kumwezesha mwanafunzi huyu kushiriki vyema katika elimu ya msingi ambayo itatekelezwa kwa kipindi cha miaka saba. Utekelezaji umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni katika kipindi kisichozidi miaka mitatu. Katika sehemu hii mtaala rekebifu umejikita katika kumjengea mwanafunzi mwenye uziwikutoona umahiri katika utumiaji wa stadi za mawasiliano na utumiaji wa stadi za kujimudu. Aidha, ukuzaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) utafanyika ndani ya miaka mitatu ya mwanzo kulingana na uwezo wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona. Sehemu hii ni nyumbufu kwani imeandaliwa kwa kuzingatia kuwa miaka ya mwanzo ya kujifunza kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona ni muhimu sana katika kujenga stadi za kujimudu, ujifunzaji katika darasa jumuishi na makuzi ya mtoto kiakili, kimwili na kijamii. Kwa mwanafunzi atakayemudu stadi stahiki katika sehemu hii atajumuishwa katika Mtaala wa Elimu ya Msingi ambapo atajiunga darasa la tatu katika mfumo wa elimu jumuishi katika elimu ya msingi. Aidha, mwanafiunzi ambaye ataonekana kutomudu stadi stahiki ataendelea na sehemu ya pili ya mtaala rekebifu wa elimu ya msingi.

Lengo kuu kwa sehemu ya pili ya mtaala huu ni kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona kujenga stadi za ujasiriamali, sanaa na michezo na TEHAMA. Aidha, ujenzi wa stadi za mawasiliano, kujimudu, na KKK zitaendelezwa kwani ni msingi muhimu katika kumjengea stadi za ujumuishaji katika jamii atakayoishi. Ni matarajio yetu kuwa mtaala huu, utatekelezwa kwa ushirikiano baina ya sekta ya umma, binafsi na wadau wa maendeleo ya elimu. Aidha, mtaala huu rekebifu utahusisha makundi yote ya wanafunzi wenye uziwikutoona.

# Mambo Yaliyozingatiwa katika Uandaaji wa Mtaala

## Utangulizi

Mtaala huu rekebifu, umezingatia mahitaji maalumu ya mwanafunzi mwenye uziwikutoona katika utoaji wa elimu ya msingi ili kufikia umahiri uliokusudiwa. Aidha, mtaala huu unalenga kuendeleza umahiri utakaojengwa na mwanafunzi mwenye uziwikutoona kutoka upimaji wa hatua moja kwenda nyingine. Hivyo, katika kila hatua kutakuwa na ujuzi na maarifa kwa yale ambayo mwanafunzi amejifunza katika hatua iliyotangulia. Vilevile, kutakuwapo na ufuatiliaji wa karibu wa utendaji wa mwanafunzi mmojammoja katika kila hatua ili kuhakikisha umahiri uliokusudiwa kujegwa umefikiwa. Pia, mtaala huu umeandaliwa kwa kuzingatia sheria na sera ya elimu, pamoja na matamko ya kimataifa na kitaifa yanayohusu haki za watu wenye ulemavu.

## Matamko ya Kimataifa kuhusu Utoaji wa Haki ya Elimu kwa Watu wenye Ulemavu

### Tamko la Salamanka la mwaka 1994

Mtaala huu rekebifu, umezingatia tamko la Salamanka la Mwaka 1994 linalohusu elimu kwa watoto wenye ulemavu. Watoto wenye ulemavu wana haki ya kufurahia na kupata elimu kama watoto wengine. Tanzania imesaini na kuridhia maazimio ya tamko hili linalolenga katika utoaji wa huduma mbalimbali zikiwamo huduma za kielimu kwa haki na usawa. Tamko hili linaendana na Tamko la Haki za Watu wenye Ulemavu la Mwaka 2006 na Mkataba wa Haki za Mtoto wa Mwaka 1989. Tamko la Salamanka linahimiza nchi zote kutoa elimu kwa watu wote kwa kuzingatia mahitaji yao. Msisitizo umewekwa kwenye elimu kwa wote katika mazingira jumuishi. Shule zenye mrengo wa ujumuishi zina ufanisi katika kuondoa ubaguzi na kujenga jamii jumuishi kwa watoto wenye uziwikutoona.

### Kongamano la Dakar kuhusu elimu kwa wote la mwaka 2000

Mtaala huu rekebifu umezingatia tamko la Dakar la mwaka 2000 linalohusu elimu kwa wote. Katika kongamano hilo ilibainika kuwa nchi nyingi zilikuwa zimepiga hatua kufikia malengo yaliyowekwa katika Mkutano wa Kimataifa wa Elimu kwa Wote Mwaka 1990. Washiriki walikubaliana kuhusu Mfumo wa Utekelezaji wa Dakar na kubainisha malengo muhimu ya elimu ambayo yanalenga kukidhi mahitaji ya ujifunzaji wa watoto wote, wakiwamo watoto wenye ulemavu ifikapo mwaka 2015.

### Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu wa Mwaka 2006

Mkataba huu unasisitiza kuwa, watu wote wenye ulemavu wako sawa mbele ya sheria na wanalindwa na sheria bila ubaguzi wowote. Ibara ya 24 ya mkataba huu, inabaininisha haki ya kielimu kwa watu wenye ulemavu. Kwa mujibu wa ibara hii, hakuna mtu au taasisi

itakayozuia udahili wa watu wenye ulemavu kwa sababu zozote zile zikiwamo changamoto za uziwikutoona. Watu wenye ulemavu wana haki ya kupata elimu na mafunzo katika mazingira jumuishi. Hivyo, wanafunzi wenye uziwikutoona wana haki sawa ya kupata elimu kama watoto wengine.

## Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030

Mtaala huu rekebifu umezingatia malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia ya mwaka 2030. Malengo yanahusu , pamoja na mengine utoaji wa elimu bora ili kuondoa matabaka kwenye elimu na kuhakikisha upatikanaji wa elimu katika ngazi zote ikiwamo mafunzo ya ufundi stadi kwa watu wanaoishi katika mazingira hatarishi hususani, wenye ulemavu. Vilevile, lengo hili linasisitiza kuhakikisha kunakuwapo elimu bora na jumuishi, na kuongeza fursa ya elimu endelevu kwa wote wakiwamo wanafunzi wenye uziwikutoona.

## Matamko ya Kisera

### *Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014*

Mtaala huu rekebifu, umezingatia Sera ya Elimu ya mwaka 2014 ambayo imeweka msisitizo mkubwa katika kuhakikisha kuwa kila mtoto anapata elimu ya awali kabla ya kupata elimu ya msingi. Katika utoaji wa elimu ya msingi msisitizo zaidi umewekwa katika ujenzi wa stadi za Kuandika, Kusoma na Kuhesabu (KKK) katika miaka miwili ya elimu ya msingi. Azma kuu katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 ni kujenga msingi imara wa elimu kwa wanafunzi nchini ambao hutegemea sana upatikanaji wa stadi hizo. Watoto wanapoimarishwa vyema katika stadi za KKK humudu vyema masomo yao shuleni. Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 mkazo umewekwa katika utoaji wa elimu maalumu. Mtazamo huu umewekwa ili kukidhi mahitaji maalumu ya wanafunzi wakiwamo wanafunzi wenye ulemavu. Sera hii inasisitiza ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa elimu pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya elimu ya msingi. wakiwamo wanafunzi wenye ulemavu. Sera hii inasisitiza ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa elimu pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya elimu ya msingi.

### *Sera ya Taifa kuhusu Ulemavu ya Mwaka 2004*

Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo (wakati huo), kwa kutambua umuhimu wa utoaji wa huduma na afua stahiki kwa watu wenye ulemavu nchini iliandaa Sera ya Taifa ya Watu wenye Ulemavu ya Mwaka 2004. Pamoja na masuala mengine, sera inasisitiza kuwa watoto wenye ulemavu watapewa kipaumbele katika kupata elimu kwa kuondoa changamoto za kimfumo, kimtazamo na kimazingira. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, elimu humpa mtoto mwenye ulemavu nafasi ya kujiendeleza na hivyo kumwezesha kumudu mazingira na kujipatia maendeleo. Hivyo, Mtaala Rekebifu wa Elimu ya Msingi kwa

Mwanafunzi mwenye Uziwikutoona unatekeleza azma ya serikali ya kutoa fursa sawa za elimu kwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule, wakiwamo watoto wenye uziwikutoona.

### *Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu wa Miaka Mitano (2016 - 2021)*

Mtala huu rekebifu, umezingatia mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu ambao unalenga kuimarisha umiliki na ushirikiano katika usimamizi na utoaji wa elimu ya msingi katika ngazi ya jamii. Aidha, mpango huo umelenga kushughulikia changamoto muhimu za tasnia ya elimu kwa kuzingatia uimarishaji na uhusiano ndani ya sekta ya elimu kwa ujumla.

### *Mkakati wa Elimu Jumuishi (2018 - 2021)*

Mtaala huu rekebifu, umezingatia Mkakati wa Elimu Jumuishi wa Mwaka 2018/2021 ambao umebaini uwapo wa hali inayoweza kufanikisha utekelezaji wa lengo la nne la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG 4) hapa Tanzania. Uwapo wa sera ya elimu bila ada (Sera ya Elimu na Mafunzo, 2014) kwa mwanafunzi wa elimumsingi (elimu ya msingi na miaka minne ya mwanzo ya elimu ya sekondari), na Mkakati Jumuishi wa Kitaifa na sera ya jinsia inathibitisha msimamo imara wa Tanzania kutekeleza SDG 4 na 5, Ajenda ya Elimu 2030 na Mkakati wa Elimu wa Bara la Afrika (CESA). Mikakati hii inatoa fursa zaidi kwa kuharakisha mafanikio katika sekta ya elimu Tanzania kwa kulenga hasa ujumuishi na utoaji wa fursa ya haki sawa katika sekta ya elimu. Kutenga na kuweka vipaumbele kwa elimu ya awali, elimu ya wasichana, watoto wenye mahitaji maalumu na watoto walio nje ya mfumo rasmi wa elimu itasaidia kukabiliana na ukosefu wa haki sawa pamoja na kupunguza umaskini. Mkakati huu, unatilia mkazo katika utoaji wa fursa sawa za elimu kwa watoto wote, wakiwamo watoto wenye uziwikutoona.

## Sheria ya Elimu Namba 25 ya Mwaka 1978

Mtaala huu rekebifu, umezingatia maelekezo ya Sheria ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978 na marekebisho yake Sura ya 353 ya mwaka 2002 ambayo inalinda haki ya mtoto ya kupatiwa elimu. Sheria inaeleza wazi kuwa elimu ya msingi ni ya lazima kwa watoto wote. Aidha, sheria hii inasisitiza kwamba kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule ataandikishwa shule na kuhudhuria kwa muda wote anaotakiwa kuwa shuleni bila kukosa. Kanuni zinazohusika na sheria hii zinahesabu kuwa ni kosa kwa mzazi/mlezi atakayeacha kumwandikisha shule mtoto mwenye umri wa kwenda shule.

## Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya Mwaka 2010

Sheria ya watu wenye ulemavu Na. 9 ya mwaka 2010 inalinda na kutetea haki za watu wenye ulemavu Tanzania Bara. Haki hizo ni pamoja na kupata elimu, ajira, huduma za afya, mawasiliano na miundombinu fikivu. Sheria inabainisha kupatikana kwa haki hizi bila ubaguzi. Aidha, vifungu vya 27, 28 na 29 katika sheria hii vinaelekeza kumpa elimu mtoto mwenye ulemavu katika mazingira jumuishi au maalumu yanayozingatia upatikanaji wa walimu wataalamu, mbinu fikivu za mawasiliano, vifaa saidizi, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, teknolojia saidizi na utambuzi wa mapema wa mtoto mwenye ulemavu. Mtaala huu rekebifu umeandaliwa kwa kuzingatia sheria ya watu wenye ulemavu ili kutoa fursa sawa kwa mtoto mwenye uziwikutoona kupata elimu itakayomwezesha kujitegemea na kushiriki katika shughuli za kila siku katika jamii inayomzunguka.

## Kiunzi cha Mtaala wa Taifa kwa Elimumsingi na Elimu ya Ualimu

Uandaaji wa Mtaala Rekebifu wa Elimu ya Msingi kwa Mwanafunzi mwenye Uziwikutoona umezingatia mambo muhimu yaliyopo katika kiunzi cha Taifa cha Mtaala wa Elimumsingi na Elimu ya Ualimu cha mwaka 2019. Kiunzi hicho kimekuwa msaada mkubwa katika uandaaji wa mtaala huu rekebifu kwa kuwa umetaja waziwazi umuhimu wa uwapo wa elimu maalumu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Aidha, kiunzi kimeonesha umuhimu wa uwapo wa mtaala unaozingatia mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu, wakiwamo wanafunzi wenye uziwikutoona. Kiunzi kimesisitiza kuwezesha wanafunzi wenye mahitaji maalumu kujenga stadi zinazowasaidia katika kushiriki shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kimaendeleo. Hivyo, kiunzi cha Mtaala cha Taifa kinasisitiza shule za msingi kuwajumuisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya ujifunzaji. Masuala ya kujenga stadi na ujuzi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu yatafanyika endapo shule na vyuo vinakuwa msaada na sehemu salama ya kupata mahitaji yao ya kielimu.

## Mitazamo ya Mtaala Rekebifu kwa Mwanafunzi mwenye Uziwikutoona

Uandaaji wa Mtaala Rekebifu wa Elimu ya Msingi kwa Mwanafunzi mwenye Uziwikutoona umejikita katika mitazamo mbalimbali kama vile; mtaala unaozingatia falsafa ya elimu, utamaduni, lugha, sayansi na teknolojia pamoja na elimu jumuishi. Mtaala huu rekebifu ambao unamgusa moja kwa moja mwanafunzi mwenye uziwikutoona, utaweka mazingira mazuri ya kumtambua na kumpa haki ya elimu mwanafunzi mwenye uziwikutoona. . Aidha, mtaala huu rekebifu umefafanua umahiri mkuu na umahiri mahususi ambao unampa dira mwalimu ili kumwezesha mwanafunzi kujifunza stadi za KKK kwa ufanisi na kufikia

malengo yaliyokusudiwa. Mtaala huu ni rekebifu kwa kuwa umezingatia makundi ya wanafunzi wenye uziwikutoona walioandikishwa katika shule za msingi. Katika makundi ya wanafunzi wenye uziwikutoona wapo ambao watamudu stadi zote za hatua ya kwanza na ya pili na kujumuishwa katika elimu ya msingi katika madarasa jumuishi kuanzia Darasa la Tatu. Kwa wale ambao hawatamudu stadi zilizoainishwa katika Hatua ya I na Hatua ya II wataendelea kutumia mtaala huu rekebifu kwa muda wa miaka minne wakitekeleza Hatua ya III ya mtaala huu.

## Malengo ya Elimu ya Msingi

Mtaala huu rekebifu umezingatia malengo yaliyoainishwa katika Kiunzi cha Mtaala cha Taifa kwa Elimumsingi kwa kuzingatia mahitaji ya ujifunzaji ya wanafunzi wenye uziwikutoona.

### *Malengo ya Elimu Tanzania*

a) Kuelekeza na kukuza maendeleo, kuboresha haiba ya wananchi wa Tanzania, rasilimali zao na matumizi bora ya rasilimali hizo katika kuleta maendeleo ya mtu binafsi na ya kitaifa.

b) Kukuza tabia ya kuthamini utamaduni, mila na desturi za watu wa Tanzania;

c) Kukuza upatikanaji wa fursa za kusoma, kuandika na kuhesabu na matumizi sahihi ya maarifa na stadi za kijamii, kisayansi, kiufundi, kiteknolojia, kitaalamu na aina nyingine za maarifa na ujuzi, kwa ajili ya maendeleo na kuboresha hali ya mtu na jamii;

d) Kukuza na kuendeleza kujiamini, kudadisi, weledi na kuheshimu utu wa mtu na haki za binadamu na kuwa tayari kufanya kazi kwa kujiendeleza na kwa maendeleo ya taifa;

e) Kuwezesha na kupanua mawanda ya kujipatia maarifa, kuboresha na kukuza stadi za kiakili, kivitendo, uzalishaji na nyingine zinazotakiwa katika kukidhi mabadiliko ya mahitaji kiuchumi;

f) Kumwezesha kila raia kuelewa misingi ya katiba ya nchi pamoja na kuthamini haki za binadamu na uraia, wajibu na majukumu yanayoendana nayo;

g) Kukuza utashi wa kupenda na kuheshimu kazi za kujiajiri na kuajiriwa na kuboresha utendaji kazi katika sekta za uzalishaji na huduma;

h) Kujenga misingi ya maadili yanayokubalika kitaifa na ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na sheria kwa njia ya kujifunza; na

i) Kuwezesha kuwapo kwa matumizi sahihi, usimamizi na utunzaji wa mazingira.

## Malengo ya Jumla ya Elimu ya Msingi

a) Kumwezesha kila mwanafunzi kuelewa na kuthamini utu wake, kujipatia maarifa, kuheshimu na kuthamini asili ya utamaduni wetu, mila na desturi za jamii, pamoja na umoja wa Kitaifa, utambulisho, maadili na kujiamini;
b) Kutoa fursa ya kumwezesha kila mwanafunzi kupata maarifa, kuthamini na kutumia kikamilifu lugha ya Kiswahili na kuiheshimu kwa kuwa ni alama ya umoja, utambulisho na heshima ya taifa;
c) Kumwezesha kila mwanafunzi kufahamu misingi ya katiba ya nchi pamoja na kuheshimu haki za binadamu na uraia, wajibu na majukumu ya kila raia;
d) Kumwezesha kila mwanafunzi kupata zana za msingi za kujifunzia kusoma na kuandika, mawasiliano, kuhesabu na kutatua matatizo pamoja na misingi ya kujifunza maarifa mchanganyiko, ujuzi na mwelekeo unaohitajika ili kumudu maisha na maendeleo kwa kadiri ya uwezo wake;
e) Kumpa mwanafunzi misingi ya kujitegemea, kujiendeleza na kujiamini;
f) Kumwandaa mwanafunzi kwa ajili ya ngazi ya pili ya elimu yaani elimu ya sekondari, ufundi stadi na elimu endelezi; na
g) Kumwandaa mwanafunzi kuingia katika ulimwengu wa kazi.

## Malengo ya Elimu Maalumu

a) Kumpunguzia mwanafunzi mwenye ulemavu athari za ulemavu alizonazo kwa kumpatia mafunzo rekebishi mapema iwezekanavyo;
b) Kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona kujenga stadi ambazo zitamfanya aweze kuendesha maisha yake kwa kujitegemea na kujiamini;
c) Kumwezesha mwanafunzi mwenye ulemavu kushiriki kikamilifu katika shughuli za familia/jamii anamoishi;
d) Kumpatia mwanafunzi mwenye ulemavu nafasi ya kujiendeleza kitaaluma kadiri ya uwezo wake; na
e) Kuendeleza na kukuza vipaji vya wanafunzi wenye ulemavu

## Malengo ya Elimu kwa Wanafunzi wenye Uziwikutoona

a) Kumjengea mwanafunzi uwezo wa kutumia stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu, kutamka maneno, kutumia Breli na Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT);
b) Kumjengea uwezo wa kuwa huru kihisia, kujiendeleza na kujiamini awapo nyumbani, shuleni na katika jamii;

c) Kukuza ujuzi na maarifa kwa mwanafunzi utakaomwezesha kujitegemea kupitia mafunzo ya ufundi sahili;
d) Kukuza ujuzi kwa mwanafunzi utakaomwezesha kujenga tabia na mitazamo ili aweze kuchangamana na jamii;
e) Kumjengea mwanafunzi stadi za ujasiriamali;
f) Kumjengea mwanafunzi ujuzi wa kutumia TEHAMA;
g) Kukuza uwezo wa kutambua na kutetea haki zake za kikatiba;
h) Kukuza ari ya kuthamini na kutunza mazingira; na
i) Kukuza uwezo wa kutumia stadi za mawasiliano katika jamii.

## Walengwa wa Mtaala

Mtaala huu rekebifu umeandaliwa kwa kuwalenga wanafunzi wenye uziwikutoona ambao wamegawanyika katika aina tano (5):

a. Uziwikutoona kabisa;
b. Uziwi na uoni hafifu;
c. Uziwi hafifu na kutoona kabisa;
d. Uziwikutoona wastani; na
e. Uziwikutoona wenye ulemavu mwingine.

Mtaala huu rekebifu unaweza kutumiwa na wadau wengine wa elimu kama vile; wakufunzi wa vyuo vya ualimu, wathibiti ubora wa shule, maofisa elimu wa wilaya, maofisa elimu, elimu maalumu wa halmashauri, maofisa elimu kata, wasaidizi wa walimu, wazazi, walezi, watafiti, walimu wa wakuu na walimu wanaofundisha wanafunzi wenye uziwikutoona.

# Mchakato wa Uandaaji wa Mtaala

## Utangulizi

Kazi ya kuandaa mtaala hupitia katika hatua mbalimbali ili kupata mtaala ambao unakidhi mahitaji ya walengwa. Mtaala huu rekebifu umeandaliwa kwa kufuata ule wa Elimu ya Msingi wa mwaka 2019 ambao ulipitia hatua mbalimbali ili kuhakikisha kuwa mtaala huu unagusa maeneo muhimu yanayohusu ujifunzaji wa wanafunzi wote wakiwamo wanafunzi wenye uziwikutoona. Aidha, mchakato wa uandaaji huu wa mtaala rekebifu umeshirikisha wadau mbalimbali wa elimu wakiwamo wazazi, jamii, sekta ya umma na sekta binafsi na asasi za kiraia. Lengo la ushiriki wa wadau ni kuhakikisha kuwa mtaala unabeba mambo muhimu yanayogusa jamii hasa kwa wanafunzi wenye uziwikutoona.

## Hatua za Kuandaa Mtaala

### Tathmini ya uhitaji

Hatua hii ilihusisha kukusanya maoni ya wadau kuhusu utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye uziwikutoona. Kati ya mwaka 2008 na 2013 Shirika la Sense International (EA) Tanzania kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania walifanya utafiti kuhusu ujifunzaji wa wanafunzi wenye uziwikutoona walioandikishwa katika shule za msingi. Utafiti huo ulionesha umuhimu wa kuwa na mtaala rekebifu ambao utakidhi mahitaji ya ujifunzaji wa wanafunzi wenye uziwikutoona. Matokeo ya tafiti hizo yalikuwa ni kuandaliwa kwa Kisawidi cha "Muhtasari wa Masomo ya Elimu ya Msingi kwa Wanafunzi Viziwi wasioona" mwaka 2013. Uandaaji wa kisawidi hicho ulichangiwa na utekelezaji wa Mkakati wa Elimu Jumuishi wa Mwaka 2009-2017 uliolenga kuhakikisha kuwa watoto, vijana na watu wazima wanapata fursa sawa ya elimu katika mazingira jumuishi.

Mwaka 2020, shirika lisilo la kiserikali la Sense international (EA) Tanzania lilifanya utafiti ili kubaini uwezo wa shule zilizoandikisha wanafunzi wenye uziwikutoona katika kuwezesha ujifunzaji. Utafiti huo ulishirikisha WyEST, OR-TAMISEMI, wathibiti ubora, maofisa elimu, elimu maalumu wa wilaya, wakuu wa shule, walimu wanaofundisha katika madarasa ya wanafunzi wenye uziwikutoona, walimu mwega, na wakufunzi wa Chuo cha Ualimu - Elimu Maalumu Patandi. Utafiti ulibaini changamoto za kutokuwapo mtaala na vifaa vyake katika uwezeshaji wa ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wenye uziwikutoona. Wakati wa uandaaji wa mtaala huu, matokeo ya tafiti, miongozo ya ufundishaji katika darasa jumuishi, na taarifa za utekelezaji wa elimu jumuishi na elimu kwa wanafunzi wenye uziwikutoona yalichambuliwa kwa kina na baadhi ya mapendekezo, yalijumuishwa katika

uandaaji wa mtaala huu. Aidha, matokeo ya utafiti yalionesha ni ya muhimu na kusisitiza uandaaji wa mtaala wa ujenzi wa umahiri kwa wanafunzi wenye uziwikutoona.

Maoni na mapendekezo yaliyokusanywa mwaka 2019 yaliyohusu utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Msingi wa Mwaka 2005 yalihusisha wadau mbalimbali wakiwamo walimu 300 kutoka mikoa 24 ya Tanzania Bara. Aidha, wadau wengine wa elimu walionesha uhitaji wa kuzingatia utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye uziwikutoona. Vilevile, taarifa na tafiti mbalimbali nchini zinaonesha uhitaji wa kuzingatia mahitaji maalumu katika utoaji wa elimu ya msingi nchini ikiwa ni pamoja na Kiunzi cha Mtaala wa Taifa kwa Elimumsingi na Elimu Ualimu cha mwaka 2019.

## Mikutano ya wadau kuhusu utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye uziwikutoona

Mikutano ya wadau katika utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye uziwikutoona imekuwa ikifanyika kwa ufadhili wa Shirika lisilo la kiserikali la "Sense International" tangu mwaka 2008 ikihusisha serikali, wazazi wa watoto wenye uziwikutoona, watu wenye uziwikutoona, wawakilishi wa vyama vya wanafunzi wenye uziwikutoona, chama cha wazazi wenye watoto wenye uziwikutoona, walimu, na mashirika yanayotoa huduma za elimu kwa watoto wenye ulemavu imeonesha changamoto katika utekelezaji wa elimu jumuishi. Mikutano hiyo, imeonesha kutokuwapo kwa mitaala rekebifu na inayokidhi mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu wakiwamo wanafunzi wenye uziwikutoona.

## Majopo ya wataalamu wa elimu maalumu

Katika mikutano ya jopo la wataalamu wa elimu maalumu iliyoratibiwa na TET kuanzia mwaka 2003 hadi 2010, ilibainika kuwa kuna upungufu katika utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye uziwikutoona, ambapo walimu wanakosa mihtasari ya kufundishia shuleni. Kutokana na hali hiyo, jopo la wataalamu lilipendekeza TET iandae muhtasari rekebifu wa elimu ya msingi kwa wanafunzi wenye uziwikutoona.

Katika kutekeleza mapendekezo ya wanajopo, TET kwa kushirikiana na "Shirika lisilo la kiserikali la "Sense International (EA) Tanzania" walifanya utafiti wa uhitaji wa muhtasari kwa wanafunzi wenye uziwikutoona. Matokeo ya utafiti yalikuwa ni TET kuandaa kisawidi cha Muhtasari wa Masomo ya Elimu ya Msingi kwa Wanafunzi Viziwiwasioona. Kisawidi kiliwasilishwa kwa wanajopo wa jopo la wataalamu wa elimu maalumu ambalo lilifanyika mwaka 2013 ili kupitia na kutoa mapendekezo. Kisawidi kiliandaliwa kwa kuzingatia maudhui yaliyolengautekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Msingi wa Mwaka 2005.

Kutokana na mabadiliko ya mtaala unaozingatia maudhui kwenda katika mtaala unaozingatia ujenzi wa umahiri wa mwaka 2016. TET iliitisha jopo la wataalamu ili kuandaa Mtaala Rekebifu wa Elimu ya Msingi kwa Mwanafunzi mwenye Uziwikutoona mwaka 2021 ili kupitia maoni na mapendekezo ya wadau, na Kisawidi cha Muhtasari wa Masomo ya Elimu ya Msingi kwa Wanafunzi Viziwiwasioona kwa lengo la kuandaa mtaala unaozingatia ujenzi wa umahiri.

## Ushiriki wa wazazi na jamii

Wazazi na walezi wa watoto wenye uziwikutoona walishirikishwa katika utafiti uliofanywa na TET na shirika lisilo la kiserikali la “Sense International (EA) Tanzania” mwaka 2010 na kutoa maoni katika kuandaa mtaala huu. Wazazi na walezi hao walishirikishwa kwa njia ya mahojiano yaliyofanyika majumbani mwao. Pia, mahojiano yalishirikisha:

a) Maofisa elimu, elimu maalumu kutoka WyEST;
b) Walimu wakuu wa shule za msingi;
c) Walimu wanaofundisha wanafunzi wenye uziwikutoona;
d) Wanafunzi wenye uziwikutoona;
e) Wahudumu; na
f) Mashirika yanayojishughulisha na utoaji wa huduma kwa watoto wenye uziwikutooona.

Utafiti mwingine ulifanywa na TET, kwa ajili ya kuandaa moduli za mafunzo kabilishi kwa walimu kazini wanaotoa afua stahiki katika ujifunzaji katika madarasa jumuishi mwaka 2020. Utafiti huo ulibaini kuwa walimu hawakuwa na mitaala, mihtasari na miongozo katika ufundishaji wa elimu ya msingi katika madarasa maalumu na jumuishi. Maoni na mapendekezo waliyoyatoa yalitumika katika kuandaa mtaala huu.

## Ubia kati ya Serikali na sekta binafsi

Sekta ya Elimu ni eneo muhimu la uwekezaji kwa njia ya ushirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Mtaala huu rekebifu umeandaliwa na TET kwa ufadhili wa “Sense International (EA) Tanzania”.

# Umahiri katika Mtaala Rekebifu wa Elimu ya Msingi kwa Mwanafunzi mwenye Uziwikutoona

## Utangulizi

Mtaala Rekebifu wa Elimu ya Msingi kwa Mwanafunzi mwenye Uziwikutoona umezingatia maeneo makuu matano ya umahiri ambayo ni utumiaji wa stadi za mawasiliano katika jamii, utumiaji wa stadi za kujimudu, ukuzaji wa stadi za KKK, utumiaji wa stadi za ujasiriamali katika uzalishaji mali, ukuzaji wa stadi za michezo na sanaa pamoja na utumiaji wa TEHAMA katika mawasiliano. Stadi hizi zitasomwa katika hatua tatu za elimu ya msingi ambazo zinalenga kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona kupata umahiri wa kujitegemea katika maisha yake ya kila siku. Hivyo basi, maeneo haya ya kujifunza yatamjengea mwanafunzi mwenye uziwikutoona kiafya, kimwili, kiakili na kisaikolojia kwa kushiriki katika michezo, kuchora, kuimba, kuigiza na elimu ya dini ambayo ina nafasi kubwa katika kumsaidia mwanafunzi mwenye uziwikutoona kuwa na maadili. Vilevile, mtaala huu rekebifu, umeandaliwa kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri katika elimu ya msingi kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona. Mwanafunzi mwenye uziwikutoona atakayemudu stadi stahiki sehemu ya kwanza ya mtaala huu rekebifu atajumuishwa katika darasa jumuishi la elimu ya msingi. Aidha, mwanafunzi asiyemudu sehemu ya kwanza ya mtaala huu kwa kipindi cha miaka mitatu ataendelea na mtaala huu kwa kusoma Hatua ya I -III. Umahiri huo umefafanuliwa katika sehemu zinazofuata:

## Umahiri katika Sehemu ya Kwanza

Sehemu hii inaakisi Darasa la Awali, Darasa la I na Darasa la II. Katika sehemu hii ya mtaala rekebifu mwanafunzi mwenye uziwikutoona atajenga umahiri katika utumiaji wa stadi za mawasiliano katika jamii, stadi za kujimudu na stadi za KKK. Sehemu hii ya mtaala ni rekebifu hivyo, mara mwanafunzi mwenye uziwikutoona akimudu umahiri na stadi lengwa atajumuishwa katika darasa jumuishi katika shule ya msingi.

**Hatua ya I**

**Jedwali Na. 1: Utumiaji wa stadi za mawasiliano katika jamii**

| Umahiri Mahususi | Shughuli ya kutendwa na mwanafunzi |
|---|---|

| | |
|---|---|
| 1) Kutumia njia mbalimbali za mawasiliano | a. Kuonesha njia mbalimbali za mawasiliano.<br>b. Kubadilisha njia za mawasiliano kuendana na muktadha.<br>c. Kutumia njia mbalimbali za mawasiliano katika ujifunzaji |
| 2) Kutumia vifaa vya mawasiliano katika ujifunzaji | a. Kutofautisha vifaa mbalimbali vya mawasiliano<br>b. Kuwasiliana kwa kutumia vifaa mbalimbali vya mawasiliano<br>c. Kutumia teknolojia saidizi katika mawasiliano |
| 3) Kutumia stadi za kuhesabu | a) Kuhesabu vitu vilivyomo ndani na nje ya darasa kuanzia 1-99<br>b) Kufanya mazoezi ya kuongeza na kupunguza vitu kutokana na idadi aliyopewa<br>c) Kutumia matendo ya kihisabati<br>d) Kubaini maumbo mbalimbali<br>e) Kubaini nyakati na majira<br>f) Kubaini vipimo mbalimbali |

## Umahiri katika Sehemu ya Pili

Sehemu hii katika mtaala huu rekebifu ni Hatua ya III ambayo inamlenga mwanafunzi mwenye uziwikutoona ambaye hatajumuishwa katika darasa jumuishi la shule ya msingi. Lengo la Hatua ya III katika mtaala huu rekebifu ni kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona kumudu stadi za ujumuishwaji katika shughuli mbalimbali za kifamilia, kijamii, kiuchumi, kimaadili na kimaendeleo ili kutoa mchango na kushiriki vyema katika kujenga uchumi binafsi, jamii na kwa maendeleo ya taifa. Hatua ya III imebeba umahiri unaolenga kujenga stadi za utumiaji wa stadi za ujasiriamali katika kazi za ujasiriamali, michezo na sanaa na utumiaji wa TEHAMA katika mawasiliano. Mtaala Rekebifu kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona umejikita katika umahiri ambao utamwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona katika hatua ya III kumudu umahiri ufuatao:

**Jedwali Na. 2: Utumiaji wa stadi za ujasiriamali katika uzalishaji mali**

| Umahiri | Shughuli za kutendwa na mwanafunzi |
|---|---|
| 1. Kutumia mafunzo kabilishi | a) Kutofautisha uelekeo kwa kutumia sehemu za mwili wake<br>b) Kubaini uelekeo katika mazingira<br>c) Kubaini alama za kudumu na zisizo za kudumu |
| 2. Kutumia mbinu za ujongeaji | a) Kubaini mbinu mbalimbali za ujongeaji<br>b) Kutumia mbimu za ujongeaji<br>c) Kutumia mbinu za kujilinda wakati wa ujongeaji katika mazingira aliyopo. |
| 3. Kumudu stadi za kujitegemea | a) Kubaini sehemu za mwili wa binadamu<br>b) Kubaini vifaa vya usafi wa mwili wake<br>c) Kuonyesha uwezo wa kufanya usafi wa mwili wake<br>d) Kuonyesha uwezo katika stadi za kujitegemea |
| 4. Kushiriki katika shughuli za kijamii | a) Kubaini alama za taifa<br>b) Kufafanua alama za taifa<br>c) Kubaini muundo wa uongozi katika ngazi mbalimbali<br>d) Kubaini vitendo vya unyanyasaji na udhalilishaji |
| 5. Kujikinga na magonjwa mbalimbali | a) Kubaini aina za magonjwa<br>b) Kufafanua dalili za magonjwa mbalimbali<br>c) Kuchambua njia za kujikinga na magonjwa mbalimbali |

**Hatua ya pili**

**Jedwali Na. 3: Ukuzaji wa stadi za KKK**

| Umahiri Mahasusi | Shughuli za kutendwa na mwanafunzi |
|---|---|
| 1. Kutumia stadi za kusoma katika mawasiliano | a) Kubaini irabu, konsonanti na silabi<br>b) Kutamka irabu, konsonanti, silabi, neno na sentensi fupi<br>c) Kuumba irabu na konsonanti<br>d) Kuunda silabi, neno na sentensi fupi<br>e) Kusoma neno, sentensi na habari fupi kwa kuzingatia alama za uandishi<br>f) Kusimulia matukio na hadithi mbalimbali. |
| 2. Kutumia stadi za kuandika | a) Kutengeneza vifani vya maumbo ya irabu na konsonanti<br>b) Kuandika irabu, konsonanti, silabi, neno, maneno na sentensi fupi kwa kutumia vifaa vya kuandikia<br>c) Kuandika habari fupi kwa kufuata alama za uandishi. |
| 3. Kutumia stadi za kuhesabu | a) Kuhesabu vitu vilivyomo ndani na nje ya darasa kuanzia 1-99<br>b) Kufanya mazoezi ya kuongeza na kupunguza vitu kutokana na idadi aliyopewa<br>c) Kutumia matendo ya kihisabati<br>d) Kubaini maumbo mbalimbali<br>e) Kubaini nyakati na majira<br>f) Kubaini vipimo mbalimbali |

## Umahiri katika Sehemu ya Pili

Sehemu hii katika mtaala huu rekebifu ni Hatua ya III ambayo inamlenga mwanafunzi mwenye uziwikutoona ambaye hatajumuishwa katika darasa jumuishi la shule ya msingi. Lengo la Hatua ya III katika mtaala huu rekebifu ni kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona kumudu stadi za ujumuishwaji katika shughuli mbalimbali za kifamilia, kijamii, kiuchumi, kimaadili na kimaendeleo ili kutoa mchango na kushiriki vyema katika kujenga uchumi binafsi, jamii na kwa maendeleo ya taifa. Hatua ya III imebeba umahiri unaolenga kujenga stadi za utumiaji wa stadi za ujasiriamali katika kazi za ujasiriamali, michezo na sanaa na utumiaji wa TEHAMA katika mawasiliano. Mtaala Rekebifu kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona umejikita katika umahiri ambao utamwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona katika hatua ya III kumudu umahiri ufuatao:

**Jedwali Na. 4: Utumiaji wa stadi za ujasiriamali katika uzalishaji mali**

| Umahiri Mahususi | Shughuli ya kutendwa na mwanafunzi |
|---|---|
| 1. Kueleza dhana ya ujasiliamali na uzalishaji mali | a) Kufafanua dhana ya ujasiriamali na uzalishaji mali<br>b) Kueleza sifa za mjasiriamali<br>c) Kubaini shughuli za uzalishaji mali |
| 2. Kutumia nyenzo za ujasiriamali katika uzalishaji mali | a) Kubaini nyenzo za uzalishaji mali<br>b) Kuchambua nyenzo za uzalishaji mali<br>c) Kutumia teknolojia saidizi katika shughuli za uzalishaji mali<br>d) Kubaini mbinu za kupata nyenzo za uzalishaji mali |
| 3. Kubuni miradi ya uzalishaji mali | a) Kubaini hatua za uzalishaji mali<br>b) Kuonesha maadili ya uzalishaji mali<br>c) Kuanzisha shughuli za uzalishaji mali<br>d) Kutatua changamoto za uzalishaji mali |

**Jedwali Na. 5: Ukuzaji wa stadi za michezo na sanaa**

| Umahiri Mahususi | Shughuli ya kutendwa na mwanafunzi |
|---|---|
| 1. Kuchezamichezo sahili | a) Kufanya mazoezi ya viungo<br>b) Kucheza michezo sahili kulingana na umri na mazingira husika<br>c) Kucheza michezo ya jadi<br>d) Kucheza mpira<br>e) Kushiriki katika riadha. |
| 2. Kumudu kazi za sanaa na ufundi | a) Kuchora picha za vitu mbalimbali, maumbo, herufi, namba, kupaka rangi na kutia nakshi<br>b) Kufinyanga vitu mbalimbali<br>c) Kuumba maumbo ya vitu mbalimbali kwa kutumia makunzi yanayopatikana katika mazingira yao. |
| 3. Kuimba nyimbo kwa kutumia ala za muziki | a) Kuimba nyimbo mbalimbali<br>b) Kutumia ala za muziki<br>c) Kuimba nyimbo kwa kutumia ala za muziki |
| 4. Kumudu sanaa za maonyesho | a) Kuigiza matukio<br>b) Kusimulia hadithi mbalimbali<br>c) Kuigiza vitendo vya kuchekesha<br>d) Kucheza ngoma mbalimbali |

**Jedwali Na. 6: Utumiaji wa TEHAMA katika mawasiliano**

| Umahiri mahususi | Shughuli ya kutendwa na mwanafunzi |
|---|---|
| 1. Kubaini vifaa vya TEHAMA | a) Kubaini vifaa vya TEHAMA<br>b) Kueleza matumizi ya vifaa vya TEHAMA<br>c) Kuchukua hadhari za matumizi ya TEHAMA |
| 2. Kutumia TEHAMA katika maisha ya kila siku | a) Kutumia huduma za mtandao katika mawasiliano<br>b) Kuzingatia maadili katika matumizi ya TEHAMA<br>c) Kutumia programu andishi<br>d) Kutumia programu jedwali |
| 3. Kutunza vifaa vya TEHAMA | a) Kuchunguza kanuni za maabara za TEHAMA<br>b) Kuonesha sehemu mbalimbali za kutunza vifaa vya<br>c) TEHAMA<br>d) Kueleza umuhimu wa kutunza vifaa vya TEHAMA |

## Umahiri katika Stadi Wezeshi

Eneo la stadi wezeshi limejikita katika kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona kujenga umahiri katika stadi za kuwasiliana, kujimudu, na stadi za KKK. Jedwali Na. 7 linaonesha uwezo wa kutenda ambao mwanafunzi anatarajiwa kuujenga katika Hatua ya I na Hatua ya II.

**Jedwali Na. 7: Umahiri katika stadi wezeshi Hatua ya I**

| Kutunza afya na mazingira | Kujiendeleza katika michezo na sanaa |
|---|---|
| Kubaini sehemu za nje za mwili wa binadamu | Kucheza michezo sahili |
| Kuwasiliana katika jamii | Kuwasiliana na kujimudu katika michezo |
| Kubaini njia za kujikinga na magonjwa | Kuonesha mwenendo sahihi katika michezo |
| Kutunza mazingira | Kufuata kanuni katika michezo na sanaa |
| Kutoa huduma ya kwanza | Kuwasiliana kupitia sanaa |
| Kutambua viumbe hai | Kubuni na kuimarisha stadi za michezo na sanaa |

## Elimu ya Dini na Maadili

Mtaala huu rekebifu, utahusisha pia elimu ya dini na maadili. Elimu hii inahusika katika kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona kujenga imani, tabia ya uadilifu, uvumilivu na kuheshimu tofauti za kiimani na kiitikadi wakati wote na mahali popote. Hivyo, kutakuwa na vipindi vya dini na maadili kila wiki. Vilevile, kwa wanafunzi wa madhehebu yanayoabudu siku ya Ijumaa, nafasi itatolewa kwa wanafunzi kushiriki ibada kati ya saa 6 na saa 8 mchana. Muda huo, hakutakuwa na vipindi vyovyote na wanafunzi wengine watatumia muda huo kujisomea.

## Muda wa Kufundisha na Idadi ya Vipindi

Mwaka wa masomo utakuwa na siku 194 ambazo ni sawa na wiki 39. Mwaka umegawanywa katika mihula miwili; hivyo kutakuwa na mihula miwili (2) ya masomo. Katika kila muhula wiki mbili (2) zitatumika kwa upimaji. Ili kufikia malengo ya mtaala huu rekebifu na kupata matokeo yanayotarajiwa, mwanafunzi wa Hatua ya I atajifunza utumiaji wa stadi za mawasiliano katika jamii na utumiaji wa stadi za kujimudu. Katika Hatua ya II atajifunza stadi moja ya ukuzaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Aidha, katika Hatua ya III atajifunza ukuzaji wa stadi za sanaa na michezo, utumiaji wa stadi za ujasiriamali katika uzalishaji mali na utumiaji wa TEHAMA katika mawasiliano. Muda wa kufundisha kwa wiki ni saa 15 na kutakuwa na vipindi (6) kwa siku. Muda wa kila kipindi utakuwa wa dakika 30 tu. Hivyo, katika siku moja ya mafunzo itampasa mwanafunzi mwenye uziwikutoona kujifunza kwa muda wa saa 3 tu. Mgawanyo huu wa vipindi na saa za masomo utategemea pia uwezo wa mwanafunzi na kiwango cha ulemavu alichonacho ambapo saa zinaweza kuongezeka au kupungua kutokana na shughuli anayoifanya kwa wakati huo.

# Ufundishaji na Ujifunzaji

## Utangulizi

Mtaala huu rekebifu, umezingatia mtazamo wa Mtaala wa Elimu ya Msingi wa kujifunza ambao unasisitiza mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji. Kutokana na mtazamo huu jukumu la mwalimu ni kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona kujifunza. Kila mwanafunzi mwenye uziwikutoona ana uwezo wa kujifunza, hivyo huhitaji msaada wa mwalimu kurahisisha ujifunzaji huo. Mtaala huu rekebifu unasisitiza matumizi ya mbinu shirikishi katika utekelezaji wake. Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji katika mbinu shirikishi humpa mwalimu fursa za kutenda na kushirikisha wanafunzi wote bila kujali tofauti zao. Mtazamo huu wa ufundishaji na ujifunzaji umejikita katika falsafa ya Elimu ya Kujitegemea.

## Vitengo, Madarasa Maalumu na Madarasa Jumuishi

Serikali inaweka mkazo katika kutoa elimu bora kwa wanafunzi wote wa Tanzania kupitia elimu jumuishi. Aina hii ya elimu, inatambua kuwa kila mwanafunzi anaweza kujifunza na kufanikiwa. Mtaala huu rekebifu unabainisha mambo ya kuzingatia katika kuhama kwa mwanafunzi kutoka katika kitengo au darasa maalumu la wanafunzi wenye uziwikutoona kwenda darasa jumuishi katika shule ya msingi. Kwa mwanafunzi ambaye atabainika kuwa na uziwikutoona akiwa katika darasa jumuishi atahamishiwa kwenye kitengo ili kujenga stadi za mawasiliano, kujimudu na KKK kama hakuzipata vyema, na akimudu atarudishwa kwenye darasa jumuishi. Mwanafunzi ambaye atakuwa katika kitengo au darasa maalumu la wanafunzi wenye uziwikutoona asiyemudu stadi za Hatua ya I na Hatua ya II atabakia kwenye kitengo au darasa maalumu na kuendelea na Hatua ya III hadi kumaliza elimu ya msingi kwa kutumia mtaala huu rekebifu.

## Shughuli katika Mtaala wa Ziada

Shughuli katika mtaala wa ziada, zitafanyika kwa lengo la kuimarisha maarifa na stadi ambazo mwanafunzi mwenye uziwikutoona amejifunza ndani ya darasa. Hii itamwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona kuchangamana na wanafunzi wengine pamoja na mazingira ya nje ya darasa. Muktadha huu huimarisha ujenzi wa maana kwa yale anayojifunza. Shughuli hizo zitajumuisha klabu za masomo na maeneo mengine ya kujifunza. Vilevile; zitakuwapo shughuli za michezo, uzalishaji mali, utamaduni, malezi na unasihi. Shughuli hizi zitawezesha wanafunzi kujifunza kwa kina. Ufuatao ni ufafanuzi wa shughuli katika mtaala wa ziada:

(a) **Klabu za masomo**

Klabu hizi zitahusisha masomo mbalimbali na klabu za masuala mtambuko. Hizi zitajumuisha klabu za mazingira, VVU na UKIMWI, jinsia na haki za mtoto. Pia, kutakuwa na klabu za stadi za maisha, kupinga/kudhibiti rushwa, afya, uelimishaji rika, biashara na usalama barabarani.

(b) **Uzalishaji mali**

Wanafunzi wenye uziwikutoona watajifunza shughuli mbalimbali za uzalishaji mali shuleni. Madhumuni yake ni kujifunza stadi za ujasiliamali. Shughuli hizo ni kama kuendesha duka la shule na kulima bustani za mboga au maua. Vilevile, watafanya shughuli za ufugaji, maigizo, uimbaji, ufinyanzi, ususi, uchongaji, uchoraji na biashara ndogondogo.

(c) **Burudani**

Wanafunzi mwenye uziwikutoona watafanya shughuli za kuburudisha mwili na akili wakiwa shuleni. Shughuli anuai zikiwamo ziara na matamasha zitafanyika mara moja kwa muhula.

Kila shule itaainisha na kupanga shughuli za burudani zitakazoshirikisha wanafunzi wote. Hii itakuza usawa na ushirikiano miongoni mwa wanafunzi wenyeuziwikutoona. Motisha itatolewa kila hatua kwa watakaofanikiwa zaidi ili kuwapa ari ya kuendeleza vipaji vyao. Mtaala huu umelenga kufikia mafanikio yafuatayo kutokana na kuendeleza burudani shuleni:

i) Kuibua vipaji na ubunifu wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona
ii) Kuendeleza vipaji binafsi vya mwanafunzi mwenye uziwikutoona kama ile; kuigiza, kucheza muziki, kuimba na kucheza michezo mbalimbali
iii) Kuwezesha wanafunzi wenye uziwikutoona kuburudisha akili na miili yao; na
iv) Kukuza ari binafsi ya mwanafunzi mwenye uziwikutoona kupenda kusoma masomo mengine ya taaluma.

Mwanafunzi mwenye mwelekeo katika fani mbalimbali atasaidiana na walimu na wataalamu wengine katika usimamizi wa shughuli za burudani shuleni.

# Rasilimali katika Utekelezaji wa Mtaala Rekebifu wa Elimu ya Msingi kwa Mwanafunzi mwenye Uziwikutoona

## Utangulizi

Viwango vya rasilimali katika utekelezaji wa mtaala vimegawanywa katika makundi makuu manne. Makundi hayo ni rasilimali watu, vitu, muda na fedha.

## Rasilimali Watu

Rasilimali watu ni nguzo muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa mtaala, hususani shughuli za kufundisha na kujifunza shuleni. Rasilimali watu inajumuisha mwalimu mahiri katika kuwezesha ujifunzaji wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona na mwalimu mwega anayesaidiana na mwalimu katika kuwezesha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Mwalimu atakayetekeleza mtaala huu anatakiwa awe amepata mafunzo ya kufundisha wanafunzi wenye uziwikutoona katika ngazi hii kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali. Vile vile, mwalimu huyu anatakiwa awe na sifa za mwalimu wa Elimu ya Msingi kama zilivyofafanuliwa kwenye Kiunzi cha Taifa cha Mtaala 2019. Sifa kuu za mwalimu wa ngazi hii ni kuwa mahiri katika kuwezesha mchakato wa ufundishaji, upimaji na tathmini.

Sifa za mwalimu na mwalimu mwega zimebainishwa katika sehemu zifuatazo

## Sifa za mwalimu wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona

a) Uelewa stahiki wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona;
b) Uelewa katika kuandaa mpango binafsi wa ujifunzaji wa mwanafunzi mwenye uziwi kutooona;
c) Uelewa wa njia na mbinu za kufundishia na kujifunzia mwanafunzi mwenyew uziwikutoona;
d) Uelewa katika mbinu na njia za mawasiliano kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona;
e) Uelewa katika uwezeshaji wa mafunzo kabilishi na ujongeaji kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona;
f) Uelewa katika kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia zinazozingatia mahitaji ya mwanafunzi mwenye uziwikutoona;
g) Uelewa katika kuandaa na kutumia zana za upimaji kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona;

h) Uelewa katika teknolojia saidizi kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona;
i) Uelewa katika kutunza kumbukumbu za maendeleo ya mwanafunzi mwenye uziwikutoona katika ujifunzaji kwa kila umahiri;
j) Uelewa katika kutumia matokeo ya upimaji na tathmini ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona; na
k) Uelewa katika kutoa mrejesho kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona, wazazi, serikali na wadau wa maendeleo ya elimu ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

## Sifa za mwalimu mwega wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona

a) Awe na uelewa kuhusu mwanafunzi mwenye uziwikutoona;
b) Awe na uwezo wa kuwasiliana kulingana na mfumo wa mawasiliano wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona;
c) Awe na uwezo wa kumsaidia mwanafunzi wakati wa mchakato wa ujifunzaji;
d) Awe na uwezo wa kumsaidia mwanafunzi mwenye uziwikutoona katika kushirikiana na wadau wa elimu;
e) Awe na stadi za kuwezesha kujenga stadi za kujimudu kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona;
f) Awe mwenye uvumilivu kwani atakaa na mwanafunzi muda wote hata baada ya mafunzo ya darasani; na
g) Awe na uwezo wa kufaragua zana kwa ajili ya mwanafunzi mwenye uziwikutoona.

## Rasilimali Vitu

### Samani na miundombinu

Ikumbukwe uandaaji wa samani na miundombinu yote ya shule inapaswa izingatie viwango vilivyowekwa na WyEST. Hivyo, shule inatakiwa kuwa na:

a) **Majengo:** Jengo la utawala, madarasa maalumu kwa ajili ya wanafunzi wenye uziwikutoona, bwalo la chakula na kumbi za mikutano zenye vifaa wezeshi vinavyoendana na idadi ya wanafunzi kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi wenye uziwikutoona.
b) **Maabara**: Kuwapo na maabara za kutosha zenye wahudumu wenye sifa stahiki kwa masomo ya Sayansi na Teknolojia. Pia, maabara ziwe na vifaa saidizi kwa ajili ya wanafunzi wenye uziwikutoona na ziwe na ofisi za walimu.
c) **Nyumba za wafanyakazi:** Ziwepo nyumba za kutosha zenye viwango vya ubora kwa ajili ya wafanyakazi zinazozingatia mahitaji maalumu.
d) **Vyanzo vya nishati:** Shule iwe na vyanzo.

e) **Vibaraza na njia za miguu zilizofunikwa:** Shule iwe na vibaraza na njia zinazopitika kiurahisi na zenye mazingira fikivu kwa wanafunzi wenye uziwikutoona.

f) **Huduma za maktaba:**

   i) Kuwe na maktaba ya kisasa ya TEHAMA yenye vifaa vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia vinavyozingatia mahitaji maalumu;

   ii) Kuwe na maktaba na wakutubi mahiri;

   iii) Kuwe na huduma ya intaneti na tovuti ya shule; na

   iv) Kuwe na vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye uziwikutoona.

g) **Vyombo vya usafiri:** Kuwe na vyombo vya usafiri vya kuaminika kwa ajili ya wanafunzi vinavyokidhi mahitaji ya wanafunzi wenye uziwikutoona.

h) **Karakana:** Shule iwe na karakana ya matengenezo ya vifaa mbalimbali inayokidhi mahitaji ya wanafunzi wenye uziwikutoona.

i) **Miundombinu ya huduma za afya na usalama:** Shule inayoandikisha mwanafunzi mwenye uziwikutoona ni budi kuwa na huduma za afya, ikiwa ni pamoja na vyoo, mfumo wa majitaka, maji safi na salama, mafunzo ya usafi na usalama, vifaa vya zimamoto, huduma ya kwanza na huduma za zahanati zinazozingatia mahitaji ya wanafunzi wenye uziwikutoona.

j) **Viwanja na maeneo ya michezo na burudani:** Shule inayoandikisha mwanafunzi mwenye uziwikutoona ni budi kuwa na viwanja vya michezo na maeneo ya kutosha ya michezo ya ndani na nje pamoja na vifaa vya kutosha vya michezo na burudani vinavyozingatia mahitaji ya wanafunzi wenye uziwikutoona.

k) **Mabweni:** Shule inayoandikisha mwanafunzi mwenye uziwikutoona ni budi kuwa na mabweni yenye viwango vinavyokubalika kwa kuzingatia miundombinu fikivu kwa ajili ya wanafunzi wenye uziwikutoona. Aidha, mabweni yawe na vyoo vya kutosha vinavyozingatia mahitaji ya wanafunzi wenye uziwikutoona.

## Vifaa vya kufundishia na kujifunzia

Shule iwe na vifaa vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia vinavyozingatia mahitaji maalumu ya mwanafunzi mwenye uziwikutoona vikiwamo:

a) Vitabu vya kiada na ziada

b) Vitabu vya rejea

c) Viongozi vya walimu

d) Zana za kufundishia

e) Vifani

f) Matini mbalimbali ya kusoma
g) Chati ya mgawanyo wa vipindi vya kufundisha
h) Chatipindu
i) Televisheni
j) Projekta
k) Kompyuta na vifaa vyake
l) Mbao za kuandikia
m) Kamusi za lugha ya alama
n) Vitabu vyenye maandishi yaliyokuzwa
o) Vitabu vya maandishi ya breli
p) Vifaa vya kuandikia maandishi ya breli kama vile "Perkins Braller"
q) Vifaa vya upimaji kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona
r) Vifaa saidizi kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona
s) Vifaa vya sanaa na michezo
t) "Orbit reader 20"

## Rasilimali Muda

Muda wa utekelezaji wa Mtaala Rekebifu wa Elimu ya Msingi kwa Mwanafunzi mwenye Uziwikutoona ni miaka saba. Kila mwanafunzi atapaswa kujifunza kwa wiki 273 sawa na siku 1365 kwa miaka saba. Muda huu utatumika ili kufikia umahiri uliokusudiwa.

## Rasilimali Fedha

Utekelezaji wa Mtaala Rekebifu wa Elimu ya Msingi kwa Mwanafunzi mwenye Uziwikutoona unategemea rasilimali fedha kutoka serikalini. Aidha, wadau wengine watashiriki katika utekelezaji wa mtaala huu.

# Upimaji wa Maendeleo ya Mwanafunzi Mwenye Uziwikutoona

## Utangulizi

Upimaji ni sehemu muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji utamwezesha mwalimu kubaini kufikiwa kwa ujenzi wa umahiri uliokusudiwa. Upimaji utafanyika kwa kutumia zana mbalimbali zikiwamo mitihani ya kuandika, uchunguzi makini, mahojiano, maswali ya ana kwa ana, mkoba wa kazi na orodha hakiki. Upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi utahusisha upimaji wa; awali, endelevu, gunduzi, chekeche na upimaji tamati. Upimaji endelevu utatoa mrejesho kwa mwalimu na mwanafunzi ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji tamati utahusisha pia upimaji wa hatua ya III ambao utampa mwalimu mwanga wa kumpa afua stahiki na kuupangia mkondo sahihi kutokana na uwezo wake. Yafuatayo ni maelezo kuhusu upimaji utakaofanywa kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona.

## Upimaji wa Awali

Upimaji wa awali utafanyika kabla ya mafunzo ili kupima kiwango cha uelewa na umahiri alionao mwanafunzi kabla ya mafunzo rasmi. Upimaji huu utafanywa mara tu mwanafunzi mwenye uziwikutoona anapofika shuleni. Lengo lake ni kumwezesha mwalimu kutambua mahitaji binafsi ya mwanafunzi. Mahitaji hayo atayatumia kuandaa mpango binafsi wa kielimu na mipango ya kuwawezesha watoa huduma wengine kufikia malengo yaliyokusudiwa. Upimaji huu pia unaweza kutumika katika kuwapanga wanafunzi katika makundi kwa kuzingatia mahitaji yao. Shule zinatakiwa ziwe na utaratibu wa kuwapima wanafunzi wenye uziwikutoona kabla ya kuanza masomo katika Hatua ya I.

## Upimaji Gunduzi na Majaribio Chekeche

Upimaji huu ni sehemu ya upimaji endelevu. Upimaji huu utafanyika ili kupata taarifa kuhusu uwezo wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona katika kumudu stadi mbalimbali. Taarifa za upimaji zitatumika kutoa ushauri na msaada stahiki kwa wanafunzi wenye changamoto za ujifunzaji. Wakati fulani msaada wa mtaalamu wa afya unaweza kuhitajika hasa kwa watoto wenye uziwikutoona. Pamoja na upimaji gunduzi, majaribio chekeche au mitihani chekeche itatumika. Lengo lake ni kuwabaini wanafunzi wenye changamoto katika kujifunza stadi mbalimbali ili kuandaa mpango binafsi wa kielimu.

## Upimaji Endelevu

Upimaji huu utafanyika wakati wote wa ufundishaji na ujifunzaji ili kutoa mrejesho kwa mwalimu na mwanafunzi. Mrejesho utamwezesha mwalimu kuelewa maeneo yenye changamoto ambayo yanahitaji kutiliwa mkazo. Zana za upimaji zitakazotumika ni pamoja na uchunguzi makini, mahojiano, mazoezi, maswali ya ana kwa ana, mkoba wa kazi na mtihani wa kuandika. Upimaji huu pia, utatumika kubaini vipaji mbalimbali vya mwanafunzi mwenye uziwikutoona kama ubunifu, uchoraji, sanaa na michezo. Aidha, utahusisha mitihani ya mwisho ya mihula ambayo itawezesha kubaini uwezo wa mwanafunzi katika stadi mbalimbali.

## Upimaji Tamati

Upimaji huu utafanyika mwisho wa kila mwezi na muhula. Mtihani wa mwisho utatumika kama kigezo cha wanafunzi kutoka ngazi moja kwenda nyingine. Aidha, upimaji huu utapaswa uzingatie kiwango cha uwezo wa utendaji wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona. Upimaji huu utahusisha mtihani wa kuandika, maswali ya ana kwa ana na uchunguzi makini.

## Upimaji wa Kitaifa

Kutakuwa na upimaji wa kitaifa mwisho wa Hatua ya II ambao ni sawa na Darasa la II. Upimaji huu utaandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania na ratiba yake itakuwa moja kwa nchi nzima. Baraza la Mitihani la Tanzania litatoa matokeo ya upimaji ya nchi nzima na yatatumika katika shule husika ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Ufuatiliaji wa usimamizi na usahihishaji utafanywa na maofisa wa Baraza la Mitihani la Tanzania pamoja na maofisa kutoka maeneo mengine yanayohusika na usimamizi wa elimu ya msingi kwa wanafunzi wenye uziwikutoona. Aidha, upimaji wa kitaifa kwa hatua ya II utatumika kubaini kama mwanafunzi amefikia umahiri uliotarajiwa ili avuke ngazi moja kwenda ngazi nyingine (yaani kutoka hatua ya pili kwenda darasa la III) katika shule jumuishi. Kwa wale wasiomudu stadi za Hatua ya I na Hatua ya II wataendelea na ujifunzaji katika Hatua ya III ya mtaala huu.

Upimaji wa kitaifa mwisho wa Hatua ya II utakuwa na lengo la jumla la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Hivyo, upimaji huu hautakuwa wa mchujo bali utatumika kubaini kiwango cha utendaji wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona kulingana na umahiri uliokusudiwa. Matokeo ya upimaji huu yatatumika kuandaa mpango wa kuwasaidia wanafunzi wenye uziwikutoona watakaobainika kuwa na changamoto katika ujifunzaji.

Zana mbalimbali za upimaji zitakazotumika ni kama orodhahakiki, majaribio, maswali ya kuandika, kusoma na hojaji.

# Usimamizi wa Mtaala

## Usimamizi wa Mtaala

Usimamizi wa mtaala ni jambo muhimu katika kuhakikisha unatelekezwa kama ulivyokusudiwa. Usimamizi wa utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Msingi kwa Mwanafunzi mwenye Uziwikutoona utafanyika kuanzia ngazi ya shule hadi wizara. Vilevile, usimamizi utakwenda sambamba na utoaji wa mafunzo endelevu kwa watekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mtaala husika.

## Majukumu ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa

Usimamizi wa utekelezaji wa Mtaala Rekebifu wa Elimu ya Msingi kwa Mwanafunzi mwenye Uziwikutoona utafanyika kuanzia ngazi ya shule hadi wizara. OR-TAMISEMI ndiyo msimamizi mkuu wa utekelezaji wa mtaala huu kupitia idara ya elimu. Usimamizi katika ngazi ya shule ni nguzo kuu katika utekelezaji wa mtaala. Walimu wakuu, kamati za shule, maafisa elimu kata na maofisa elimu, elimu maalumu wa halmashauri watakuwa ndiyo wasimamizi wakuu katika ngazi hii. Hivyo, kwa kupitia vikao watajadili maendeleo ya utekelezaji wa mtaala husika. Wakurugenzi wa majiji, manispaa au halmashauri ya wilaya na halmashauri ya miji kupitia maofisa elimu wa wilaya na maofisa elimu, elimu maalumu watasimamia mtaala huu katika ngazi ya wilaya. Pia, maofisa elimu wa mikoa watasimamia utekelezaji wa mtaala katika ngazi ya mikoa.

## Mafunzo Endelevu ya Mtaala kwa Watekelezaji

Walimu, wasimamizi, wathibiti ubora wa shule na vyuo, maofisa elimu, elimu maalumu pamoja na wadau wengine wa Mtaala Rekebifu wa Elimu ya Msingi kwa Mwanafunzi mwenye Uziwikutoona, watapatiwa mafunzo yatakayowawezesha kutekeleza mtaala huu kwa ufanisi. TET itandaa na kuendesha mafunzo hayo ambayo yatatolewa ana kwa ana. Vilevile, vyuo vya ualimu na vyuo vikuu vinavyoandaa walimu wa ngazi hii ya elimu vitakuwa na jukumu la kufundisha walimu tarajali kuhusu mtaala huu wa wanafunzi wenye uziwikutoona.

## Ufuatiliaji wa Upimaji wa Mtaala Rekebifu kwa Mwanafunzi mwenye Uziwikutoona

Ufuatilaji wa utekelezaji wa mtaala unalenga kukusanya taarifa kuhusu ufanisi wa mtaala. Wadau wote wa elimu watahusika katika kufuatilia utekelezaji wa mtaala wakiwamo wazazi, wajumbe wa kamati za shule, walimu, wanafunzi, maofisa elimu, elimu maalumu

na wathibiti ubora wa shule na vyuo. Wafuatiliaji hawa wamegawanyika katika makundi mawili; wafuatiliaji wa ndani na wafuatiliaji wa nje. Walimu wakuu ni wafuatiliaji wa ndani na wa mwanzo wa utekelezaji wa mtaala akishirikiana na kamati ya uthibiti ubora ngazi ya shule. Miongozo ya ufuatiliaji na tathmini ya mitaala ya wizara zitakazohusika na elimu itatoa maelezo ya majukumu ya kila mdau katika kuhakikisha mtaala unatekelezwa kwa ufanisi. Taarifa za ufuatiliaji zitachambuliwa na kupelekwa TET na kwa wadau wakuu wengine wa elimu ambapo zitatumika katika mikakati ya kuimarisha utekelezaji wa mtaala huo.

Upimaji wa mtaala huu rekebifu utalenga kubaini maeneo yanayohitaji kuboreshwa. Tathmini huangalia mambo yote yaliyo katika mtaala. Mambo haya hujumuisha malengo na umahiri uliokusudiwa, maudhui na njia za kufundishia na kujifunzia. Mengine ni upatikanaji wa vifaa na zana za upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi mwenye uziwikutoona, uwezo wa walimu katika kumfundisha mwanafunzi mwenye uziwikutoona na mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Tathmini endelevu na tamati za mtaala zitafanyika kwa kuhusisha wadau mbalimbali wakiongozwa na TET. Tathmini endelevu itafanyika muda wote wa ufundishaji na ujifunzaji wakati tathmini tamati itafanyika kila mara baada ya kukamilika kwa mzunguko wa elimu ya msingi kwa wanafunzi wenye uziwikutoona.